TANGAZO LA SERIKALI Na. 109 la tarehe 14/2/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA. 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA NISHATI KWA AJILI YA UJENZI WA MRADI WA UMEME JUA KISHAPU – SHINYANGA WA MW 50 YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye gari moja linaloingizwa Nchini na Wizara ya Nishati kwa ajili ya Ujenzi wa Mradi wa Umeme jua Kishapu Shinyanga MW 50 ya mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 19 Desemba, 2024.

Msamaha

**2**. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari moja lililoainishwa kwenye jedwali, linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Nishati kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa Umeme jua Kishapu Shinyanga MW 50 umesamehewa.

Masharti

**3**. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa matumizi tofauti au litahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

**4**. Amri hii itakoma kutumika tarehe 18 Machi, 2025

JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Injini | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Prado TXL 2 8L AUTOMATIC, diesel, Colour Grey | 9056464 | 01 | JTEBR3FJ20K291469 | limeingizwa |

Dodoma
3 Januari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*